

## Habari kwa Familia - Swahili

### Nini maana ya Shindano la Kusoma la Gavana?

Shindano la Kusoma la Gavana ni mpango husikaji wa kusoma ambao ulianzishwa na Gavana mwaka 2004 ili:

- Kuhimiza wanafunzi kusoma vitabu vingi na kufurahia kusoma
  - Kuongeza hatua ya ujuzi wa kusoma
- Shindano linawataka wanafunzi kusoma vitabu 12 toka mwanzo wa mwaka wa shule hadi mwanzoni wa mwezi wa tisa.

### Jinsi gani waweza kujua zaidi kuhusu shindano?

Tembelea ukurasa wa wazazi na familia wa tovuti ya Gavana ya Shindano la Kusoma kwa habari zaidi na.

<http://www.premiersreadingchallenge.sa.edu.au/prc/pages/parents/families/>

Wasiliana na Maofisa wa Jamii wa DECD  
Simu: 8226 2756.

Wasiliana na shule ya mtoto wako.

### Vitabu gani wanafunzi wanaweza kusoma?

Wanafunzi wanaweza kusoma kutoka listi ya vitabu ya shindano la kusoma la Gavana pamoja na chaguo lao wenyewe. Listi ya vitabu inapatikana katika tovuti ya shindano la kusoma la Gavana. Wanafunzi wanaweza kuchagua kusoma vitabu katika lugha zingine mbali na Kiingereza.

- Kuanzia wanafunzi wa mwaka wa 7 wanachagua walau vitabu 8 kutoka listi ya vitabu ya Shindano la Kusoma la Gavana kwenye tovuti na vitabu vinne vya chaguo lao wenyewe.
- Wanafunzi wa mwaka wa 8 na 9 huchagua walau vitabu vine kutoka kwenye listi ya vitabu ya Shindano la Kusoma la Gavana na vitabu nane vya chaguo lao wenyewe.
- Wanafunzi wa mwaka wa 10, 11 na 12 huchagua vitabu 12 vya chaguo lao wenyewe.

### Wapi vitabu vinapatika?

Vitabu vinapatikana mashuleni, maktaba za jumua, maduka ya vitabu na kwenye tovuti za kwenye mtandao.

### Ni zawadi gani kwa anayefaulu Shindano la Kusoma la Gavana?

Cheti – mwaka wa kwanza  
Medari ya bronze – mwaka wa pili  
Medari ya almasi – mwaka wa tatu  
Medari ya dhahabu – mwaka wa nne  
Medari ya ushindi – mwaka wa tano  
Medari ya hali ya juu – mwaka wa sita  
Medari ya kupita zote – mwaka wa saba

Karatasi za Kusoma katika Maisha (R4L):  
R4L mwaka wa nane  
R4L bronze – mwaka wa tisa  
R4L almasi – mwaka wa kumi  
R4L dhahabu – mwaka wa kumi na moja  
R4L ushindi – mwaka wa kumi na mbili  
R4L juu zaidi – mwaka wa kumi na tatu  
R4L kupita zaote – mwaka wa kumi na nne

### Watu gani ni wawakilishi wa Shindano la Kusoma la Gavana?

Timu kumi na tisa za kiwango cha juu na mabalozi sita wanaunga mkono Shindano la Kusoma la Gavana. Hizi ni Klabu za Mpira ya Umoja wa Adelaide, Adelaide Lightning, Klabu ya Mpira ya Port Adelaide, Klabu ya mpira wa mkono ya hunderbirds, Mpira ya Umoja wa Adelaide na Klabu ya Kriketi ya Inge ya wanawake

### Ni wanafunzi wangapi wanahusika katika Shindano la Kusoma la Gavana?

Kila mwaka zaidi ya wanafunzi 120,000 kutoka 95% ya shule za Australia ya Kusini humaliza Shindano la Kusoma la Gavana. Wanafunzi wengi humaliza kusoma zaidi ya vitabu 12.

### Nini faida ya kuwa sehemu ya Shindano la Kusoma la Gavana?

- Kuhimiza wanafunzi wote kusoma vitabu zaidi na kufurahia kusoma zaidi
- Kuwapa wanafunzi umakini katika kusoma
- Kuongeza kujisikia nia ya mafanikio
- Kuhimiza kuhusika kwa wazazi katika kusoma kwa watoto wao.
- Kuongeza kuazima vitabu kutoka maktaba
- Kuongeza ujuzi wa kusoma.